Find this and other free educational resources at http://maktaba.tetea.org

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

MTIHANI WA TAIFA WA DARASA LA NNE

MWAKA 2006

SOMO LA KISWAHILI

054

JINA LA MTAHINIWA: .....

JINA LA SHULE: .....

WILAYA: .....

MKOA: .....

MUDA: SAA 1.00

MAELEKEZO:

1. Karatasi hii ina sehemu 5.
2. Kila sehemu ina maswali 5.
3. Majibu yote yaandikwe kwenye karatasi ya kujibia uliyopewa.
4. Andika jina lako, jina la Shule yako, Wilaya na Mkoa.
5. Simu za mkononi haziruhusiwi kwenye chumba cha mtihani.

Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner

SEHEMU YA KWANZA

IMLA

1. .....
.....

2. .....
.....

3. .....
.....

4. .....
.....

5. .....
.....

SEHEMU YA PILI

Andika neno moja linalowakilisha kundi la maneno yafuatayo:
Mf. Kuku, mwewe, kipanga, bata (ndege)

6. Kambale, changu, vibua, perege .....

7. Fenesi, embe, nanasi, chungwa .....

8. Nyanya, kabichi, mchicha, bamia .....

9. Sketi, kaptula, shati, gauni .....

10. Dawati, meza, kiti, rafu .....

SEHEMU YA TATU – METHALI

Kamilisha methali zifuatazo:

11. Kuishi kwingi .....

12. Jungu kuu .....

13. Samaki mkunje .....

14. Mchagua nazi .....

15. Wingi .....

Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner

Find this and other free educational resources at http://maktaba.tetea.org

SEHEMU YA NNE – UTUNGAJI

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia nahau iliyo sahihi kutoka katika kisanduku.

Usingizi ulipaa, fedha lukuki, walikaa chonjo, waliangua kicheko, walipigwa butwaa, walitega masikio, kufuja mali.

16. Watu wote ..... waliposikia Juma ameuawa na majambazi.
17. Wanafunzi wote ..... walipomwona mwalimu wao anacheza dansi.
18. Alikuwa na ..... lakini hakuwa na mipango mizuri ya matumizi.
19. Baada ya kuota ndoto ya kutisha ..... usiku wote.
20. Wanakijiji ..... kumsikiliza mgombea wa ubunge alipofanya kampeni yake.

SEHEMU YA TANO – UFAHAMU

Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali.

Dunia ina umbile la mviringo kama tufe. Sehemu kubwa ya tufe hilo, inayokadiriwa kuwa asilimia sabini na tano imefunikwa kwa maji ya chumvi. Sehemu hii ndiyo huitwa bahari. Hivyo maji yote ya dunia licha ya yale ya maziwa, mito, mabwawa na chemchemi ni bahari moja ambayo imegawanyika na kupewa majina mbalimbali.

Ili kurahisisha kufahamu maeneo mbalimbali, Bahari imepewa majina kwa maeneo. Maeneo hayo ni pamoja na Bahari ya Pasifiki, Bahari ya Atlantiki, Bahari ya Hindi, Bahari ya Kusini, Bahari ya Sham na Bahari ya Mediteraniani.

Tanzania imepakana na Bahari ya Hindi kwa upande wake wa Mashariki. Hii ni Bahari ambayo iko kati ya Mabara ya Afrika, Australia na Bara la Asia ambalo liko upande wa kaskazini mwa Bahari hii ya Hindi. Ukanda wa pwani ya Tanzania una urefu wa kilometa mia nane kutoka Tanga, mpakani mwa nchi ya Kenya, hadi mto Ruvuma mkoa wa Mtwara, mpakani na nchi ya Msumbiji.

Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

Find this and other free educational resources at http://maktaba.tetea.org

MASWALI

21. Sehemu kubwa ya dunia imefunikwa na:
    (a) Maji chumvi
    (b) Udongo
    (c) Hewa
    (d) Mimea

22. Kwa upande wa mashariki Tanzania imepakana na bahari ya:
    (a) Shamu
    (b) Antaktiki
    (c) Hindi
    (d) Atlantiki

23. Kichwa cha habari kinaweza kuwa:
    (a) Maji
    (b) Bahari
    (c) Maji ya baharini
    (d) Mawimbi

24. Ukanda wa pwani ya Tanzania una urefu wa kilomita .....
    (a) Mia
    (b) Nane
    (c) Mia nane
    (d) Asilimia sabini na tano

25. Maana ya tufe ni:
    (a) Kifaa kitumikacho katika michezo
    (b) Dunia
    (c) Sayari
    (d) Kitu cha mviringo mithili ya chungwa

Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner